



**KUMB: THRDC/AGM/Vol.1/2022**

**NOTISI YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA MOJA WA WANACHAMA  
(THRDC)**

Kwa wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Wanachama wa Mtandao 2022.

Ndugu Mwanachama,

**HII NI TAARIFA RASMI KWAMBA;** Mkutano Mkuu wa Kumi na Moja (11) wa Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) utafanyika wa **siku ya Jumamosi tarehe 10 mwezi wa 12** kuanzia saa nane Alasiri mpaka saa kumi na moja jioni katika ukumbi wa Kisenga – LAPF Tower Kijitonyama jijini Dar es Salaam na kwa njia ya Mtandao.

Ajenda zifuatazo zitajadiliwa:

- 1.1 Kuhakiki Akidi ya Mkutano Mkuu waliohudhuria
- 1.2 Kufungua Mkutano
- 1.3 Kuthibitisha na Kupitisha Ajenda
- 1.4 Kuidhinisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita wa mwaka 2021
- 1.5 Yatokanyo na Mkutano uliopita wa mwaka 2021
- 1.6 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya 2021
- 1.7 Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa ya mwaka 2021
- 1.8 Taarifa ya mpango kazi mwaka 2023
- 1.9 Taarifa ya mpango mkakati wa tatu wa Mtandao; 2023 – 2027
- 1.10 Mchakato wa Ununuzi na Ujenzi wa Ofisi ya Mtandao
- 1.11 Hali ya Uanachama
  - i. Kupitisha wanachama wapya
  - ii. Kufuta wanachama wanaodaiwa Zaidi ya miaka miwili kwa mujibu wa Katiba ya Mtandao
  - iii. Kuaga waratibu wa kanda waliomaliza muda wao
  - iv. Kutambulishwa kwa waratibu wapya wa kanda za Mtandao kwa miaka 2023 – 2026
- 1.12 Kufunga Mkutano.

**NOTISI HII IMETOLEWA RASMI LEO HII TAREHE 10/11/2022.** Tunategemea kupata maoni yenu kuhusu ajenda zilizopendekezwa kabla ya tarehe 25/11/2022.

Sajili ushiriki wako kupitia barua pepe [membersaffairs@thrdc.or.tz](mailto:membersaffairs@thrdc.or.tz) au namba 0743 390452 kabla ya tarehe 29/11/2022

**Ikumbukwe kwamba, Wanachama waliokamilisha vigezo vya uanachama kama inavyoeleza Katiba ndio watakaokuwa na haki ya kuhudhuria mkutano huu. Inasisitizwa kwamba, gharama za ushiriki wa mkutano huu zitagharamiwa na mwanachama mwenyewe kwa mujibu wa katiba ya Mtandao.**

Onesmo Olengurumwa

THRDC - Mratibu Kitaifa

Board of Directors:

Hon. Rtd Judge Joaquine De-Mello, Silas Nyumba, Dr. Rose Rueben, Maxence Melo, Jamila M. Juma, Hassan Kh. Juma, Edwin Soko, Edward Porokwa, Angela Benedicto.

*Defending Human Rights is not a Crime!*